



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Yah: UHUISHAJI WA LESENI ZA TAALUMA KWA WAUGUZI NA
WAKUNGA

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga inayoitwa "***The Nursing and Midwifery Act, 2010 and its regulations***".

Leseni za Uuguzi na Ukunga zipo kisheria kama ilivyoelekezwa katika **kifungu cha 21 na 38** cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga wote ambao bado hawajakamilisha zoezi la kuhuisha Leseni kwamba mnapaswa kukamilisha taratibu zote kwa kuwa ni takwa la kisheria na hatua mbalimbali zitachukuliwa kwa Wataaluma na Waajiri watakaenda kinyume na takwa hili.

Aidha, zoezi la uhakiki na maandalizi ya Leseni kwa ambao wamekamilisha taratibu kwa kuchelewa linaendelea. Hivyo, wale wote ambao wataona hawaruhusiwi kutoa huduma "***Not allowed to practice***" waingie kwenye akaunti zao binafsi za TNMCIS kwa ajili ya kufanya marekebisho yanayohitajika.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:

Jane Mazigo

Kny: MSAJILI

21. 04. 2023